HOTUBA YA MHE. Prof. MARK. J. MWANDOSYA (MB),
WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI
KWA WANANCHI WAKATI WA UZINDUZI WA MRADI WA MAJI KIJIJI
CHA MIKOMAMBA KATIKA WILAYA YA KILWA
TAREHE 9.9.2009

Mheshimiwa Said Meck Sadik, Mkuu wa Mkoa wa Lindi,
Meshimiwa Nurdin Babu, Mkuu wa Wilaya ya Kilwa,
Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas, Mbunge wa Kilwa Kusini,
Mheshimiwa Ally Mtopa, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa,
Waheshimiwa Madiwani,
Vyombo Mbalimbali vya Habari,
Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana,

Ndugu Wananchi,
Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana kwa kunipa heshima hii kubwa kuwa mgeni rasmi katika sherehe hii ya uzinduzi wa Mradi wa Maji wa Mikomamba. Kujumuika kwetu hapa kunaashiria umoja na ushirikiano mlionao katika kutatua masuala mbalimbali yanayohusu maisha yetu ya kila siku.

Ndugu Wananchi,
Serikali imeandaa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji yenye lengo la kufanikisha upatikanaji wa maji kwa kiwango cha asilimia 65 kwa umbali usiozidi mita 400 na usafi wa mazingira kwa kiwango cha asilimia 95 kwa vijijini, ifikapo mwaka 2010.

Ndugu Wananchi,
Katika kufikia azma hiyo, katika Mkoa wa Lindi, juhudi mbalimbali zimefanyika. Juhudi za hivi karibuni ni pamoja na ujenzi wa miradi ya maji ya visima virefu na chemchemi katika vijiji 33 uliofanyika kati ya mwaka 2003 na 2005 kwa msaada wa fedha kutoka Serikali ya Japan, Shirika la *Global Aid Network (GAIN)* la Canada ulioanza mwaka 2008

ambapo hadi sasa uchimbaji umefanyika katika vijiji 10, lengo likiwa ni vijiji 100. Aidha, juhudi zingine ni kupitia *Tanzania Social Action Fund (TASAF)* mfuko ambao umegharimia ujenzi wa miradi ya maji 34.

Ndugu Wananchi,

Katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, kati ya mwaka 2007/2008 na 2008/2009 miradi midogo ya ukarabati wa miundombinu imefanikisha ujenzi wa vituo vya kuchota maji vinavyokadiriwa kufikia 657 huko vijijini. Aidha, mafunzo kuhusu usafi wa mazingira na ujenzi wa vyoo bora yametolewa na shughuli za uhamasishaji zimeanza kwenye vijiji kuhusu matumizi bora ya vyoo. Jumla ya shule za msingi 144 zimehusishwa kwenye maeneo ya miradi mbalimbali. Kutokana na juhudi mbalimbali, hadi mwezi Desemba 2008, kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kwa mkoa wa Lindi ilikuwa asilimia 54.9 ikilinganishwa na wastani wa kitaifa wa asilimia 58.3.

Ndugu Wananchi,

Utekelezaji wa miradi mipya kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika mkoa wa Lindi umekwishaanza kwa Mtaalam Mshauri kutafuta vyanzo vya maji na kufanya usanifu wa ujenzi katika vijiji 10 kwa kila halmashauri. Ili kufanikisha azma hii mikakati ifuatayo imewekwa:

- Elimu zaidi kutolewa kuhusu utunzaji wa mazingira na usafi wa mwili;
- Utoaji wa elimu kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji;
- Kuhamasisha wananchi kuhusu kuchangia mifuko ya maji;
- Kuunda jumuia za kusimamia na kuendesha miradi ya maji; na
- Kutoa elimu kuhusu faida za ujenzi wa vyoo bora na vyenye gharama nafuu.

Kampuni ya ushauri iliyoshinda ambayo ndiyo imekwishaanza kazi katika halmashauri zote za mkoa wa Lindi ni Don Consult Ltd ya Tanzania.

Ndugu Wananchi,

Sera ya Maji ya mwaka 2002 imeweka wazi kuwa wadau wote wanaruhusiwa kuchangia katika utoaji wa huduma ya maji nchini. Wadau wakuu ni wananchi wenyewe, Serikali,

mashirika ya kidini, washirika wa maendeleo na sekta binafsi. Serikali inatekeleza Sera hiyo kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambapo sekta binafsi ina mchango wake katika utekelezaji wa miradi mipya au katika uendeshaji wa miradi iliyopo.

Ndugu Wananchi,

Pamoja na juhudi mbalimbali za kutoa huduma ya maji nilizoeleza hapo awali, leo hii tumekuja kushuhudia mchango wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma ya maji nchini, kupitia mradi wa maji katika kijiji cha Mikomamba.

Ndugu Wananchi,

Hapo awali, kijiji cha Mikomamba kilikuwa hakina huduma rasmi ya maji. Mwaka huu wa 2009, Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, aligharimia uchimbaji wa visima virefu vitatu. Kati ya visima hivyo, kimoja tayari kimefungwa pampu inayoendeshwa kwa umeme wa jenereta ambapo maji yanapandishwa kwenye tanki na kisha kutumika kupitia kituo cha kuchotea maji. Kisima cha pili kina maji japokuwa hakijafungwa pampu, ambapo kisima cha tatu hakina maji. Gharama za uchimbaji wa visima vyote vitatu ni takriban **shilingi milioni 36**.

Ndugu Wananchi,

Ili kuenzi mradi huu wa Mikomamba, panahitajika kusimamia uendeshaji na matengenezo yake ili kuendelea kumpa moyo Mbunge wenu. Nategemea kwamba chombo cha watumiaji maji cha kijiji kitasajiliwa na kuendeshwa na wanakijiji wenyewe katika kufanikisha lengo la Sera ya Maji la miradi ya maji kusimamiwa na kuendeshwa na wananchi wenyewe. Wote leo tunafurahi lakini tunajua ni watoto wetu na akina mama ndio wanaopata adha zaidi pindi huduma hii ya maji inapokosekana nyumbani. Natarajia kwamba akina mama ambao ndio wanapata adha sana kwa kukosekana kwa huduma hii watajitokeza kuchukua nafasi za uongozi katika chombo kitakachoundwa.

Ndugu Wananchi,

Itapita miaka mingi na inawezekana hata sisi wengi wetu tutakuwa tumetoweka duniani lakini watakaoendelea kuwepo watafundishana historia ya jinsi maji haya yalivyopatikana na historia hiyo itathamini uwepo wetu katika dunia hii, nao watakuwa na mioyo ya kutaka kuiga kutenda mema kama alivyotenda Mhe. Mbunge, maana wenye hekima walisema *mwenye haja hunena muungwana ni kitendo*, nanyi mliponena muungwana huyu alisikia akatenda kama tuanvyoona leo.Wakati mwingine huhitajika ujasiri wa kujitolea hali na mali ili kumkomboa mwanadamu, lakini leo hapa tunazungmzia kukombolewa kwa watu wengi kutokana na adha ya kupata maji katika mradi huu wa Mikomamba.

Ndugu Wananchi,

Nafanya uzinduzi nikiwa na faraja tele kwamba Mbunge wenu amejali kuwepo kwangu katika Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji na angeweza kujenga mradi huu na watu wakapata maji na mambo yakaendelea vyema na mkashiriki naye kama ilivyo siku zote, lakini aliona ni vyema atende siyo kwa kujificha bali ashirikishe jamii kama alivyotushirikisha leo na Wizara yangu itaendelea kuthamini michango ya wengi na ya mmoja mmoja hata kama ni kidogo, lakini naamini matokeo yake yanaweza kuwa ni makubwa kuliko yanavyoonekana kwa macho yetu ya kawaida. Nasema asante sana Mhe Mbunge kwa hili na watu wote wa eno la Jimbo lako la Kilwa Kusini katika kuwa mstari wa mbele kufanikisha malengo ya Taifa.

Kwa kumalizia, natoa rai kwa kwa wananchi wote mmoja mmoja au kwa vikundi, kujitolea kuchangia kwa hali na mali katika miradi ya maji. Aidha, natoa rai kwa kwa sekta binafsi kujitolea au kuchangia katika kugharamia ujenzi na pia uendeshaji wa miradi ya maji nchini.

MAJI NI UHAI

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA